

TEGEMEO TIMILIFU

By: Michael Tano
07-Aug-2014

Imba Kwa Hisia

Soprano/Alto

Tenor/Bass

Ni ta pa pa sa pa pa sa mpa ka li ni? Ni ta i shi
Ni ta wa ya wa ya mi mi mpa ka li ni? Te ge me o

S./A.

T./B.

dha mbi ni mpa ka li ni ee Ma - ma Ma ri a
ti mi li fu ni we we ee Ma - ma Ma ri a

2. Nita hangaika mimi mpaka lini? Ninategemea msaada wa..ko, ee Mama Maria.
- Nita ugulia mimi mpaka lini? Tegemeo timilifu ni we..we, ee Mama Maria.
3. Magonjwa na njaa kiu vyanitesa?, Uniombe kwa mwanao Ye...su, ee Mama Maria.
-Nipo utumwani ninahangaika?, Tegemeo timilifu ni we...we, ee Mama Maria.
4. Nipo gerezani ninahangaika?, Natamani kufika kwa mwanao, ee Mama Maria.
-Mimi ni Yatima sina pakushika?, Tegemeo timilifu ni wewe, ee Mama Maria.
5. Mimi ni Mjane kheri imekoma?, Nioneshe njia iliyo bora, ee Mama Maria.
-Maisha ya dhiki yananiandama?, Tegemeo timilifu ni wewe, ee Mama Maria.
6. Raha na karaha vinanimaliza?, Univushe katika giza nene, ee Mama Maria.
-Sina msaada sioni mwangaza?, Tegemeo timilifu ni wewe, ee Mama Maria.
7. Mimi ni Albino naishi kwa hofu?, Tumaini langu limepotea, ee Mama Maria.
-Imani potovu zanifanya mfu?, Tegemeo timilifu ni wewe, ee Mama Maria.
8. Nimtumaini nani awezaye?, Ninakimbilia ulinzi wako, ee Mama Maria.
-Mwanao Yesu ni yeye ashindaye?, Tegemeo timilifu ni we...we, ee Mama Maria.